# Ndege Mjanja

## namba shufwa na namba witiri



Age Umri 7+

Yatokana na kipindi cha TV

ubongo kids


Siku moja Kiduchu alimkimbilia Kibena na kumwambia, “Kibena njoo nikuonyeshe kitu...”



Walikimbia haraka na kukatiza msituni.



Kiduchu na Kibena wakajificha nyuma ya gogo.
Kibena akauliza, “Tunafanya nini hapa?”
Kiduchu akamjibu, “Shhh! Subiri utaona.”






“Jana niliweka mbegu na akadonoa zote. Kwa nini leo hadonoi?” Kiduchu aliuliza.

“Labda ameshiba,” Kibena alijibu.

Kibena akamwambia Kiduchu atoe mbegu moja.
Sasa kukawa na mbegu sita badala ya saba.
Ndege akadonoa zote.



Siku iliyofuata wakaweka mbegu nne,
ndege akazidonoa zote.




Siku iliyofuata Kiduchu *akapata* mbegu ishirini na mbili.





Wakagawa zile mbegu ishirini na mbili na kuweka nusu ya zile mbegu: mbegu kumi na moja. Ndege hakudonoa zile mbegu.

Kibena akamwambia Kiduchu aweke mbegu zote ishirini na mbili. Ndege akaja na kudonoa mbegu zote ishirini na mbili.






Kibena akamkimbilia ndege.
Alitaka kujua kwa nini kuna wakati fulani anadonoa mbegu na wakati mwingine hazidonoi.


Ndege akatua kwenye kiota chake.
Akaanza kuwalisha watoto wake akisema,
“Moja yako...moja yako...moja yako,”
mpaka zote zikaisha.



“Ahhh! Huyu ndege ana akili, anadonoa makundi ya mbegu yanayogawanyika kwa mbili.




Anaweza kugawanya nne katika makundi mawili.
Kila kifaranga kikadonoa mbegu mbili.




$$4 \div 2 = 2$$

Anaweza kugawanya sita katika makundi mawili.
Hivyo kila kifaranga kikadonoa mbegu tatu.



$$6 \div 2 = 3$$

Anaweza kugawanya ishirini na mbili katika makundi mawili. Hivyo kila kifaranga kikadonoa mbegu kumi na moja," alisema Kibena.




$$22 \div 2 = 11$$


“Saba na kumi na moja
hazigawanyiki kwa mbili.
Ndiyo maana hakudonoa makundi
ya saba na kumi na moja,”
Kiduchu aliongeza.




“Saba haigawanyiki kwa mbili. Unaona jinsi vifaranga vyake visingepata idadi sawa ya mbegu?” Kibena alisema.



"Vifaranga vyake vingegombania ile mbegu ya kumi na moja," alisema Kiduchu.



Yule ndege ambaye jina lake ni Mama Ndege, akawaona wale wasichana na kuwauliza kama wanapanga kuwaiba watoto wake.




“Hapana, hapana! Tunataka kujua kwa nini wakati mwingine unachukua mbegu na wakati mwingine huchukui?” Kiduchu alijibu.



"Hamuoni nina vifaranga viwili, inabidi niwape sawa sawa. Hivyo nadonoa mbegu ambazo jumla yake ni namba shufwa,"
alisema Mama Ndege.
"Namba shufwa! Ndiyo nini?"
wasichana waliuliza.



"Namba shufwa ni zile namba zinazogawanyika kwa mbili, kwa mfano: sita, nne, ishirini na mbili," Mama Ndege alijibu.



$$6 \div 2 = 3$$

$$4 \div 2 = 2$$

$$22 \div 2 = 11$$

“Vipi kuhusu namba zisizogawanyika kwa mbili, huwa zinaitwaje?” wasichana waliuliza. “Zinaitwa namba witiri kama tulivyo sisi hapa watatu,” Mama Ndege alisema.



“Tatu, saba na kumi na moja ni namba witiri,” alisema Mama Ndege.



Mama Ndege aliwashukuru watoto kwa kumpa mbegu, akapaa kwenda kuwafundisha watoto wake hisabati kwenye darasa la msituni.



# Mwisho

## Imeandaliwa na

## ubongo.co

Haki zote zimehifadhiwa.
Hairuhusiwi kupiga chapa au kukitoa kitabu hiki kwa njia ya aina yoyote bila idhini ya mwandishi, UBONGO INTERNATIONAL.